# Samia ataka ubunifu zaidi biashara TRC

**Na Selemani Nzaro**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametaka ubunifu zaidi katika kufanya biashara ya usafirishaji kwa kuboresha vitengo vya biashara na mauzo kama kuweka watu wenye weledi na ubunifu kwenye masuala ya biashara.

Rais Samia ameyasema hayo jana kwenye hafla ya kupokea mabehewa mapya na yaliyokarabatiwa pamoja na uzinduzi wa Bandari Kavu ya Kwala iliyopo wilayani Kibaha mkoani Pwani.

Alisema uzinduzi huo ni mwanzo wa safari ya nchi kuwa kitovu cha biashara kwa Kanda ya Afrika Mashariki na Kati na kwamba maendeleo hayo yanaonesha sura mpya ya Tanzania.

"Uzinduzi wa safari za treni ya mizigo ya kisasa ni ushahidi kuwa Tanzania imeamua kwa dhati kuimarisha mfumo wa usafirishaji wa mizigo kuanzia kwenye barabara, usafiri wa anga, maji na reli," alisema Rais Samia.

Aliongeza kuwa Reli ya Kisasa ya SGR kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi Dodoma ni sehemu ya mkakati wa kitaifa wa kupunguza gharama za usafirishaji, kupunguza uchakavu wa barabara na kulinda mazingira.

Alisema kwa kutumia reli hiyo mzigo unaweza kutoka bandarini na kufika Kwala ndani ya dakika 45 hadi saa moja na kufika Dodoma ndani ya saa nne hadi tano.

Alisisitiza kuwa hayo ni maboresho makubwa ya kupunguza muda unaotumiwa na magari ya mizigo ambao ni wastani wa saa 30 hadi 35 kwenda Kwala ikiwa ni pamoja na saa 24 za kukamilisha kuingia na kutoka bandarini.

"Mradi huu unatarajiwa kupunguza msongamano wa malori katikati ya Jiji la Dar es Salaam, kuongeza ufanisi wa bandari na kupunguza muda wa ushushaji na usafirishaji wa mizigo," aliongeza Rais Samia.

Alifafanua kuwa ili kuimarisha usafiri na usafirishaji wa mizigo, serikali imewekeza Sh bilioni 330 kwa ajili ya ununuzi wa mabehewa ya mizigo 1,430.

Aliiagiza Wizara ya Uchukuzi pamoja na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuhakikisha mabehewa hayo yanatumika ipasavyo katika shughuli za kibiashara.

Aliongeza kuwa kupitia mfumo wa watoa huduma binafsi, ni vyema TRC ikashirikiana na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) kama mtoa huduma binafsi ili kufikia mtandao mkubwa zaidi wa mizigo.

Alizitaka mamlaka zinazosimamia usafiri na usafirishaji wa mizigo kuendelea kuhamasisha wadau wa sekta ya usafirishaji wa ndani na nje ya nchi kuchangamkia fursa hiyo ya kutumia miundombinu hiyo ya usafirishaji kwa kununua vichwa vya treni na mabehewa yao wenyewe.

"Hii ni fursa ya biashara hivyo tutoe fursa kwa sekta binafsi wenye uwezo wa nje au ndani ya nchi kuja na mabehewa na vichwa vyao na tukubaliane namna ya kufanya kazi. Serikali kazi yake kulaza miundombinu na sekta binafsi kufanya biashara," alisema.

Kadhalika, Rais Samia aliitaka TRC kuhakikisha kuwa wawekezaji wote walioonesha nia ya uwekezaji hawakwamishwi ili kuleta ajira kwa vijana wa Kitanzania.

"Katika siku za usoni tunataka kuona mteja wa bandari popote alipo anaweza kuagiza mzigo wake kokote duniani na aweze kuchukulia Kwala kwa kutumia CIF," alisema Rais Samia.

Vilevile alisema katika mipango ya baadaye, serikali itaunganisha Kituo cha Bandari Kavu cha Kwala na Bandari ya Bagamoyo iliyopo kilometa 60 kutoka Kwala pamoja na Bandari ya Tanga iliyopo kilometa 256.

Alieleza kuwa Bandari ya Kwala ni ya Kipekee Afrika na kwamba Tanzania ni nchi ya kwanza kuwa na mradi huo Afrika Mashariki.

Alisema Kongani ya Viwanda ya Kwala itakuwa na uwezo wa kuchukua viwanda zaidi ya 200 na kutoa ajira za moja kwa moja zaidi ya 50,000 na zisizo za moja kwa moja 250,000.

Rais Samia aliishukuru Serikali ya DRC kwa kuipa Tanzania ardhi yenye ukubwa wa hekta 60 katika eneo la Kasumbalesa, Kasamboindo na Kasenga. Amezisihi nchi zote ziendeleze maeneo zilizopatiwa ili kurahisisha mifumo ya kufanya biashara kwa watu.

Kwa upande mwingine, Rais Samia alitoa maagizo mahususi kwa Wizara ya Uchukuzi na taasisi zake kuhamishia shughuli zake Kwala hadi kufika Jumatatu ya wiki ijayo.

Aidha, aliitaka wizara hiyo kuondoa msongamano wa malori yaendayo Dar es Salaam na badala yake yaishie Kwala huku akiitaka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhakikisha inajenga Kituo cha Polisi Kwala kutokana na ukubwa wa mradi huo.

Vilevile, aliitaka Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kuendelea na upanuzi wa Bandari ya Kwala ili ichukue mzigo zaidi huku akiitaka TRC kuhakikisha kunakuwa na vitengo muhimu vya utoaji wa huduma kama za usafirishaji wa mifugo na bidhaa hatarishi.

Aliitaka TRC ikamilishe Chuo cha Reli pamoja na kuboresha Chuo cha Bandari pamoja na kuyaunganisha maeneo yote na mifumo ya usafirishaji huku akisisitiza kuwa sheria zote za uzalishaji zifuatwe.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Pwani na Watanzania kwa ujumla kujiandaa kikamilifu na Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 29, mwaka huu.

# Trilioni 2.6/- kuboresha miundombinu ya usafirishaji

**Na Upendo Mosha, Kibaha**

WAZIRI wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amesema serikali imetenga zaidi ya Sh trilioni 2.6 kwa miradi ya maendeleo katika wizara hiyo hatua ambayo itasaidia uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji.

Profesa Mbarawa aliyasema hayo wakati akizungumza katika uzinduzi wa treni ya mizigo ya SGR na uzinduzi wa Bandari Kavu ya Kwala wilayani Kibaha, Pwani.

Alisema serikali imetenga zaidi ya Sh trilioni 2.6 kwa miradi ya maendeleo ambazo kati ya fedha hizo, Sh trilioni 1.11 ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya reli.

"Tunakushuru wewe binafsi (Rais Samia Suluhu Hassan) kwa kuendelea kuipatia kipaumbele sekta ya uchukuzi kwa ajili ujenzi wa miundombinu ya kisasa kama reli hii ambayo imekuwa ni kichocheo kikubwa cha uchumi katika bandari zetu," alisema Profesa Mbarawa.

Aliongeza: "Wizara yetu imepatiwa fedha nyingi ambazo zitaenda kuboresha miundombinu yetu ikiwemo viwanja vya ndege".

Aidha, alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada za muunganiko wa njia za ardhini na bandari lengo likiwa ni kupunguza msongamano bandarini na kuongeza ufanisi wa utoaji wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam.

Akizungumzia uzinduzi wa treni hiyo, alisema itakuwa na mabehewa 50 mapya na mabehewa 20 ambayo yamekarabatiwa na serikali ili kuongeza ufanisi katika usafishaji wa mizigo kati ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma.

"Sekta ya uchukuzi ni muhimu kwa maisha ya kila siku kwa raia mmoja mmoja na taifa kwa ujumla kuifanya Tanzania kufikia lengo la uchumi wa kati," alieleza.

Akizungumzia bandari hiyo, Profesa Mbarawa alisema chimbuko la ujenzi wa bandari hiyo kavu ya Kwala ilianza kwa sababu za kiuchumi, ufundi na kijamii na uwezo mdogo wa bandari kavu zilizokuwepo.

"Jiografia ya bandari hii ya Kwala ipo Vigwaza Mkoa wa Pwani ambapo ni umbali wa kilometa 15.5 kutoka barabara kuu ya Morogoro kutokea katika mizani ya Vigwaza na bandari hii ipo umbali wa kilometa 90 kutoka Bandari ya Dar es Salaam," alibainisha.

Mbali na hilo, alisema bandari hiyo ipo karibu na barabara kuu inayounganisha nchi za jirani zikiwamo Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Malawi ambazo zinatumia Bandari ya Dar es Salam kusafirisha bidhaa.

"Bandari hii inamilikiwa kwa asilimia mia moja na serikali na eneo lilikuwa mali ya serikali ambapo hatukuwa migogoro ya fidia jambo lililoharakisha mradi kukamilika haraka," alieleza.

Alisema bandari hiyo ina uwezo wa kuhudumia makasha zaidi ya 820 kwa siku na kwa mwaka ina uwezo wa kuhudumia zaidi ya makasha 300,000 ambayo ni sawa na asilimia 30 ya makasha yote yaliyokuwa yakihudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam.

"Usafirishaji wa mizigo kwa kutumia treni ya kisasa ya umeme ulianza mwaka huu kati ya Dar na Dodoma ambapo ilianza kusafirisha makasha kumi yenye zaidi ya tani 700 na Julai mwaka huu tena yalisafishwa makasha 20 yenye tani 1,400," alieleza.

Alisema bandari hiyo itasaidia kupunguza gharama za usafishaji ikiwamo kuongeza ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

CamScanner




**President Samia Suluhu Hassan pictured at the marshalling yard area at the Kwala Dry Port in Kibaha District Coast Region yesterday flagging off a train to mark the launch of cargo transportation from Dar es Salaam to Dodoma via the electric Standard Gauge Railway (SGR).** Photo: State House

# Samia: Ensure inland port gets all necessary services

**By Correspondent Julieth Mkireri, Kibaha**

ALL necessary services need to be in place at the Kwala inland container depot (ICD) within Kibaha town, 75 kilometers from Dar es Salaam port, to facilitate efficient cargo handling and ease congestion at the main port.

President Samia Suluhu Hassan issued this directive onsite yesterday in the presence of Transport minister Prof. Makame Mbarawa and heads of the various public agencies involved in the conduct of operations at the new facility.

The president specifically demanded that the Inspector General of Police move to enhance security around the facility to support safe and uninterrupted operations, where the main audience were residents of Kwala in Kibaha rural district.

She formally launched the Kwala logistics hub and standard gauge railway (SGR) freight services as well as unveiling the Kwala industrial park, expected to attract a wide range of local and international manufacturers.

The dry port and freight services are billed as a game changer in setting up a major logistics hub with direct rail links to key markets being developed at the moment, she said.

She pointed at the urgency of ensuring efficiency, transparency and stakeholder coordination across the country's logistics and transport value chain, stressing that the Kwala dry port must become fully functional, with all responsible institutions involved moving to simplify the movement of goods.

The dry port is an inland logistics hub designed to receive and dispatch cargo transported via the SGR network, part of Tanzania's broader strategy to modernise its transport infrastructure and strengthen its position as a trade gateway for East and Central Africa.

The facility is intended to ease pressure

TURN TO PAGE 2

## DK. SAMIA AZINDUA BANDARI KAVU KWALA

# Asema Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji

NA MWANAJUMA ABDI

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ameiagiza wizara ya Uchukuzi na taasisi zinazotoa huduma bandari ya Dar es Salaam, kuhamishia huduma za kibandari katika kituo cha Kwala ifikapo Agosti 4 mwaka huu.

Dk. Samia ameeleza hayo jana, kwenye hafla ya uzinduzi usafirishaji wa mizigo kwa kwa kutumia reli ya SGR, kuweka jiwe la msingi kongani la viwanda Kwala, alizindua bandari kavu Kwala na kuzungumza na wananchi.

Alisema hatua hiyo itawafanya wanaohitaji huduma hizo wakifika Vigwaza wasione ulazima kwenda Dar es Salaam kufuata huduma, wahakikishe taratibu zote zinafanyika kwa uwazi kwa kasi na uweledi.

Akizungumzia mafanikio katika banadari ya Dar es Salaam, alisema ushirikishwaji wa sekta binafsi umeongeza makusanyo kwa wastani asilimia 25 hadi asilimia 30 kwa mwaka na kiasi cha shehena kimeongezeka kutoka tani milioni 23.69 mwaka 2023 hadi tani milioni 27.76 mwaka jana.

Alisema idadi ya meli zinazohudumiwa zimepanda kutoka 1860 mwaka 2023 hadi 1990 mwaka jana, ambalo ni ongezeko la meli 130 ya mwaka mmoja na ujio wa meli kubwa zimeongezeka kutoka wastani tani 45,000 na sasa wanapokea meli za tani 65,000.

Alisema kuhamishiwa shughuli za bandari katika bandari Kavu ya Kwala, kutasaidia kuondosha msongamano wa malori kuingia Dar es Salaam ambao umekuwa kero kubwa.

Alifahamisha kuwa kufunguliwa kwa bandari ya Kwala hakutakuwa na sababu kwa gari za mizigo kuingia Dar es Salaam hasa yale yanayobeba mizigo kuingiza nchi jirani.

Alisema kituo cha Kwala kitatoa fursa kwa wafanyabiashara kutoka nchi jirani ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Zambia, Burundi na Rwanda kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi kupitia lango la Dar es Salaam.

Dk. Samia aliitaka wizara ya Uchukuzi kutengeneza mazingira mazuri kwenye bandari Kavu ya Kwala ambayo yatawezesha utoaji kwa huduma kwa ufanisi.

Alisema miradi aliyoizindua itaendelea kwa miaka mingi ijayo, hivyo shirika la Bandari na (TPA) na shirika la Banadri (TRC), kuandaa mpango wa muda mrefu wa uendelezaji wa eneo hilo la Kwala.

Sambamba na hilo, alisema kwa ukubwa wa uwekezaji ulipo katika eneo hilo aliitaka wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kuimarisha ulinzi katika eneo hilo kwa kuweka kituo cha polisi.

Alisema matukio yote matatu ya kimkakati ni mwanzo wa safari ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji wa biashara kwa kanda ya Afrika Mashariki na Kati.

Alieleza miradi hiyo mitatu itapunguza gharama kwa usafirishaji wa bidhaa kutok: na kwenda bandarini na itakuza ushindar wa Tanzania kama lango kuu la biashar: kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati kuiwezesha kushiriki kikamilifu katika enec huru la biashara la Bara la Afrika.

Akizungumzia uzinduzi wa safari reli ya mizigo ya SGR, alisema ni ushahidi kwamba Tanzania imeamua kwa dhati kuimarisha mfumo wa usafirishaji wa mizigo kuanzia katika barabara, usafiri wa anga, usafiri wa majini na katika reli ya SGR kutoka Bandar ya Dar es Salaam hadi Dodoma.

Dk. Samia alisema uznduzi wa mirad hiyo, ni sehemu ya mkakati wa kitaifa kupunguza gharaza za usafirishaji kupunguza uchakavu wa barabara na kulinda mazingira.

Alisema ili kuimarisha usafiri na usafirishaji wa mizigo, hivyo serikali imewekeza zaidi ya takribani shilingi bilioni 330 kwa ajili ya ununuzi wa mabehewa ya treni 1,430 ya mizigo ya SGR.

Kwa pande wake, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Jayaka Mrisho Kikwete alimpongeza Dk. Samia kwa kazi kubwa na mzuri anayoendelea kuifanya kwa maendeleo ya nchi yetu.

Kwa upande wake Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa alisema uzinduzi wa bandari kavu ya Kwala, safari ya treni ya mizigo ya SGR kati ya Dar es Salaam na Dodoma na upokeaji wa mabehewa ya mizigo ya treni ya kawaida 50, ni mabehewa mapya na 20 yaliyokarabatiwa.

CS CamScanner

# UDART kuundwa upya

**Na Lidya Inda**

KAMPUNI ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART) imesema imepanga kujijenga upya kimuundo ndani ya miezi 18 hadi 24 ili kuboresha huduma kwa wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa Udart, Waziri Kindamba alisema hayo Dar es Salaam kuwa ndani ya muda huo watakuwa wamekamilisha muundo huo mpya kwa kuweka utaratibu utakaohusisha wawekezaji kimkakati, serikali na wananchi kwa ujumla.

"Kama zikitokea sababu mbalimbali za kisheria na nyinginezo, tumejiwekea miaka mitatu kwa muda wa mwisho kabisa, tunaamini tutakuwa tumeshatengeneza muundo mpya wa taasisi kwa maana ya kuweka mwekezaji wa kimkakati, serikali na umma kwa ujumla," alisema Kindamba.

Alisema mabadiliko hayo yatagusa pia maeneo muhimu kama sheria zinazoongoza manunuzi, karakana, uongozi na maeneo mengine ambayo ni moyo wa taasisi.

Pia, Kindamba alisema changamoto mojawapo iliyopo kwa sasa ni kuwa mwendokasi hauna sheria kama ilivyo kwa reli na kwamba siku za mbele itakuja sheria kwa ajili ya kulinda miundombinu ya mwendokasi isiingiliwe.

Alisema kumekuwa na usimamizi usio mzuri katika muda uliopita na kwamba sasa serikali haitaruhusu tena mwekezaji binafsi kuingia kutoa huduma hizo bila kuwepo kwa mfumo mzuri wa uangalizi wa huduma na miundombinu ya mabasi hayo.

Alisema makosa ya nyuma katika usimamizi wa huduma hiyo yalichangiwa na kutokuwepo kwa mkazo katika matengenezo ya mara kwa mara ya mabasi, jambo ambalo liliathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

"Gari zile mpya zikija tutakuwa tunafanya matengenezo ya mara kwa mara kama inavyotakiwa, tunazipangia ratiba ikifika wakati wake, kilometa zile zikifika yatafanyiwa matengenezo, hayo yakifanyika hatuoni kwamba hiyo shida inaweza kutokea tena," alifafanua.

Akizungumzia basi moja lililoletwa kwa ajili ya mfano wa mengine yanayotarajiwa kuja kwa ajili ya majaribio, alisema basi moja la aina hiyo linagharimu zaidi ya milioni 500 ambayo ni sawa na Sh bilioni 50, fedha ambayo kupatikana kwake ni lazima kukopa ndiyo sababu yanaagizwa kwa awamu.

Kuhusu matumizi ya tiketi za kielekroniki, Kindamba alisema: "Bado sina taarifa rasmi kama bado watu wanatumia karatasi, inawezekana wapo mmoja, wawili kwa sababu ya nje ya utaratibu, lakini ukiniuliza kuhusu muda, hadi sasa haitakiwi mtu mzima yeyote anayeonekana kutumia karatasi kupanda mwendokasi."

Aliongeza: "Kwa sababu yapo maelekezo mahususi ya Rais kwamba mifumo isomane, malengo ya serikali ni kuunganisha data zote hakuna haja ya kuwa na kadi nyingi, mtu atatakiwa atumie kadi moja, ukienda feri, stendi ya Magufuli, uwanja wa taifa na kwingineko atumie kadi moja."

**99>>Idadi ya mabasi ya mwendokasi yanayotarajiwa kuwasili nchini Septemba mwaka huu**

# UDART yatoa mwelekeo ujio mabasi mapya mwendokasi

**NA PIUS NTIGA**

MKURUGENZI Mkuu wa Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam-(UDART), Waziri Kindamba, amesema mabasi 99 ya mwendokasi yanatarajiwa kuwasili nchini Septemba, mwaka huu.

Alisema mabasi hayo yalitakiwa kuwasili nchini mwezi ujao, lakini yatachelewa kutokana na mchakato wa ununuzi.

Mei, mwaka huu UDART ilipokea basi moja kati ya 100 kwa majaribio na kumjulisha mzalishaji kutengeneza mengine ambayo yamekamilika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kindamba alisema kuchelewa kwa mabasi hayo kunatokana na mchakato wa ununuzi serikalini ambao lazima ufuatwe.

Kindamba alisema basi lenye uwezo wa kubeba abiria 150, linauzwa sh. milioni 500, hivyo mabasi 100 zaidi ya sh. bilioni 50 zitatumika kununua.

Alisema baada ya kufanya tathimini ya basi moja linalotumia gesi, walibaini ni bora kwa kuwa linapunguza matumizi ya mafuta.

Kuwasili mabasi hayo kutasaidia kutoa ahueni ya usafiri jijini Dar es Salaam kwa njia ya Kimara-Kivukoni.

Alisema mabasi mengine yanatarajiwa kuletwa kwa kuwa UDART imekamilisha andiko la mradi na kuwasilisha Benki ya NMB ambao wameridhia kuwapa mkopo.

Alisema mabasi yatakayowasili yatakuwa na televisheni ndani kuruhusu wananchi kufuatilia mambo mbalimbali yanayoendelea nchini kupitia taarifa za habari.

"Maelekezo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ni kutatua kero ya usafiri jijini Dar es Salaam, tunatekeleza kwa vitendo kwa kuhakikisha njia zote sita za Kimara, Mbagala, Tegeta, Ubungo, Gongo la Mboto zinakuwa na mabasi ndani ya mwaka huu 2025," alisema Kindamba.

Aliwaomba wakazi wa Dar es Salaam kuwa wavumilivu wakisubiri kuwasili mabasi hayo mapya 99 yanayotumia gesi.

CamScanner